20 Kwani mlipokuwa watumwa wa thambi,
mlikuwa huru katika haki.
21 Mazao gani mliyokuwa nayo ya mambo
mliyoyatahayarikia sasa? Kwani mwisho
wao ni kufa.
22 Illa sasa mmekuwa huru katika thambi,
mkitumika na Muungu, mnayo mazao yenu
kwa kusafishwa, na mwisho uzima wa mile-
23 le. Kwani mshahara wa thambi kufa, uka-
rimu wa Muungu uzima wa milele katika
Masiya Isa Bwana wetu.
VII. Hamjui, ndugu, kwani nasema nao wai-
juao sheria, kama sheria hu'mweza mtu,
2 wakati ukiwapo hayi? Kwani mwanamke
aliyeolewa amefungwa na sheria kwa mume
akiwa hayi. Illa akifa mume, amefunguliwa
3 katika sheria yake mume. Mume akiwa
hayi, huitwa mzini, akiwa na mume mgine.
Illa mume akifa, amekuwa huru katika she-
4 ria, hatta si mzini, akiwa na mume mgine.
Hivi, ndugu zangu, mmekufa katika sheria,
kwa mwili wake Masiya, mpate kuwa ninyi
kwa mgine aliyeondoka katika wafu, mpa-
te kumzalia matunda Muungu.



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

5 Kwani tulipokuwa katika mwili, mapenzi
ya thambi zilizo kwa sheria zikatenda kati-
ka viungo vyetu, tuzae matunda kwa kufa.
6 Illa sasa tumeondoka katika sheria, tu-
meifia iliyotuweza, utumwa wetu uwe kati-
ka upya wa rohoni, si kwa ukale wa herufi.
7 Tusemeje? Sheria ndiyo thambi? Hasha.
Lakini singaliijua thambi, illa kwa sheria,
kwani singalijua kutamani, sheria isiponena,
8 Usitamani. Thambi ikipata asili kwa amri
ikatenda kwangu killa kutamani, kwani pa-
sipo sheria thambi kifu.
9 Mimi mzima kwanza pasipo sheria, ikija
amri thambi imepata uzima, mimi nikafa.
10 Nikaiona kwangu amri iliyo kwa uzima,
11 ndiyo kwa kufa. Kwani thambi ikipata
chimbuko kwa amri ikanidanganya, nikafi-
shwa nayo.
12 Hivi sheria takatifu, na amri takatifu, ye-
13 nyi haki na njema. Iliyo njema imekuwa
mauti kwangu? Hasha. Illa thambi ione-
kane kuwa thambi, ikinifanyia mauti kwalo
lililo jema, thambi iwe kwa amri na thambi
nyingi mno.



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

14 Twajua kama sheria inayo roho, nami ni
wa mwilini niliyekuzwa chini ya thambi.
15 Kwani sijui nifanyavyo, nisiyoipenda naite-
16 nda, naichukia niitendayo. Kama siipendi
niitendayo naikubali sheria kama nzuri.
17 Bassi si mimi sasa niifanyaye, illa thambi
18 ikaayo kwangu. Najua kama halikai kwa-
ngu, ndiyo mwilini mwangu, neno lililo je-
ma, kupenda ni karibu kwangu, kulifanya
19 lililo zuri sioni. Silo nilipendalo jema nili-
tendalo, lakini nisilolipenda baya ndilo nili-
20 fanyalo. Kama nisilolipenda ndilo nilifa-
nyalo si mimi tena nilifanyalo, illa thambi
ikaayo kwangu.

21 Bassi naona sheria, nipendapo kulitenda
22 lililo zuri, lililo baya karibu kwangu. Kwa-
ni napendezewa na sheria yake Muungu
23 kwa mtu wa ndani, illa naona sheria ya pili
katika viungo vyangu ikipigana nayo sheria
ya akili zangu, inifungayo katika sheria ya
thambi iliyo katika viungo vyangu.

24 Mtu maskini mimi, ni nani atakayenitoa
katika mwili wa mauti hii?

25 Namshukuru Muungu, kwa Isa Masiya



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

Bwana wetu.
Bassi nami naitumikia sheria ya Muungu
kwa akili, illa kwa mwili sheria ya thambi.
VIII. Hapana tena kuhukumiwa kwao walio
2 katika Masiya Isa. Kwani sheria yake Ro-
ho ya uzima katika Masiya Isa imenitoa ka-
tika sheria ya thambi na kufa.
3 Isiyoyaweza sheria, kwa kuwa thaifu kwa
sababu ya mwili, Muungu akimpeleka Mwa-
na wake yeye, katika mfano wa mwili wa
thambi, na kwa ajili ya thambi, amehukumu
4 thambi katika mwili, haki yake sheria itimi-
zwe kwetu, tusiokwenda kwa mwili, illa kwa
Roho.
5 Walio kwa mwili huzifikiri za mwili, wa-
6 lio kwa Roho zile za Roho. Nia yake mwili
ni mauti, nia ya Roho, uzima na amani.
7 Kwa hiyo nia ya mwili ni wadui wa Muu-
ngu, kwani haitii sheria ya Muungu wala
8 haiwezi. Walio kwa mwili hawawezi ku-
mpendeza Muungu.
9 Lakini ninyi si kwa mwili, illa kwa Roho,
kama anakaa ndani mwenu Roho ya Muu-
ngu. Mtu asiye na Roho ya Masiya, huyu



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

10 si wake. Masiya akiwa kwenu, mwili ume-
kufa kwa thambi, Roho ni uzima kwa haki.
11 Kama Roho iliyomfufua Isa katika wafu
inakaa kwenu, aliyemfufua Isa katika wafu
atafanya mizima na miili yenu kwa Roho
12 yake akaaye ndani mwenu. Bassi ndugu,
mwili hautuwii, tuufuate mwili.
13 Kwani mkifuata mwili, mtakufa, mkifisha
matendo ya mwili kwa Roho, mtakuwa hayi.
14 Kwani waifuatao Roho yake Muungu, ndio
15 waanawe Muungu. Hamkupewa roho ya
utumwa tena kwa hofu, illa mmepewa roho
ya kuwakama mwana, itulizayo, Abba, Baba.
16 Roho mwenyewe hushuhudu pamoja na roho
17 yetu kama sisi watoto wa Muungu, kama wa-
toto, warithi tena, warithi wa Muungu, wari-
thio pamoja naye Masiya, tukiwa tumeteswa
naye, tupate na kutukuzwa pamoja naye.
18 Kwani nahasibu, kama mateso ya wakati
wa sasa hayalingani na utukufu utakaofunu-
19 liwa kwetu. Kwani kutazamia sana kwake
kiumbe, kunaungoja ufunuo wao waana wa
20 Muungu. Kwani kimetiishwa na utupu ki-
umbe, si kwa moyo wake, illa kwa yule ali-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

Cambridge University Library

21 yekitiisha katika tumaini, kama nacho kiu-
mbe kitawekwa huru katika utumwa wa uha-
ribifu, kupata ungwana wa utukufu wao wa-
22 ana wa Muungu. Kwani twajua kama killa
kiumbe kinaugua, kinacho tena utungu ha-
23 ta sasa. Wala si hivyo tu, illa na sisi tulio
nao mwanzo wa Roho, na sisi tunaugua nda-
ni mwetu, tukingoja kufanyika waana, uko-
24 mbozi wa mwili wetu. Kwani tumeokoka
kwa tumaini, tumaini lililoonekana silo tu-
25 maini. Aonaye neno, mbona alitumainia?
Tukilitumaini tusiloliona twalingoja kwa
26 saburi.

Hivi na Roho huusayidia uthaifu wetu.
Kwani hatujui kutaka neno kama ilivyotupa-
sa, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa
27 kuugua kusikonenekana. Aijaribuye mio-
yo anaijua nia yake Roho kama anawaombea
watakatifu kwa Muungu.

28 Twajua kama kwao wampendao Muungu
yote huwafanyia mema, kwao walioitwa
29 kwa kusudi. Kama aliotangulia kuwajua,
akawaweka kuwa mfano mmoja na namna
ya Mwana wake, awe aliyezaliwa kwanza


Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is